# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# WIZARA YA UJENZI
# TAASISI YA TEKNOLOJIA YA UJENZI

**TANGAZO LA MAFUNZO YA KOZI YA UKARABATI NA MATENGENEZO YA BARABARA KWA KUTUMIA TEKNOLOJIA STAHIKI YA NGUVU KAZI (LABOUR BASED TECHNOLOGY)**

## 1. UTANGULIZI:

Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi (ICoT) ni Taasisi ya Wizara ya Ujenzi yenye makao yake makuu Morogoro. Taasisi inawatangazia wananchi wote kuwa inatarajia kuendesha mafunzo ya kozi ya Ukarabati na Matengenezo ya Barabara za Udongo na Changarawe kwa wadau wote wa ujenzi katika tawi la Mbeya kama ifuatavyo: -

| | Jina la kozi | Muda wa Mafunzo | Mafunzo yatafanyika |
|---|---|---|---|
| 1 | Kozi ya Ukarabati na Matengenzo ya barabara za changarawe na udongo (Gravel and Earth Road) kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi. | **Wiki kumi (10)**<br>13/04/2026– 20/06/2026 | **Mkoani Mbeya (ICoT – Mbeya)** |

## 2. MASOMO YATAKAYOFUNDISHWA:

Kozi hii, Washiriki watajifunza maada mbali mbali juu ya ukarabati na matengenezo ya barabara za udongo na changarawe kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi pamoja na maada shirikishi ambazo ni; utaratibu wa kufungua kampuni, utaratibu wa kujaza kitabu cha zabuni, Teknolojia ya Udongo na Zege Ukarabati na Matengenezo ya barabara na Usimamizi sehemu ya kazi. Kipekee, kozi hii imelenga kuwawezesha kupata ujuzi wa kufanya na kusimamia kazi za matengenezo ya barabara, yaani Matengenezo ya kawaida (Routine/Recurrent Maintenance).

## 3. NJIA ZA UFUNDISHAJI

Mafunzo yatafanyika katika awamu mbili; awamu ya kwanza itakuwa nadharia (Darasani) na awamu ya pili itakuwa ni mafunzo ya vitendo (‘Site’).

## 4. MALENGO YA KOZI

Masomo katika kozi hii yamelenga kumpatia mshiriki mbinu mbali mbali juu ya matumizi ya Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi katika:

i. Kufanya na kusimamia kazi za matengenezo ya barabara hasa matengenezo ya kawaida yaani ‘Routine/Reccurent, Periodic and Emergency maintenance’;
ii. Kufanya na kusimamia kazi za ukarabati wa barabara yaani ‘road rehabilitation’;
iii. Kuendesha na kusimamia miradi ya matengenezo na ukarabati wa barabara za vumbi/changarawe na barabara za lami;
iv. Kwa wajasiriamali, masomo haya yatawawezesha kujiajiri kwa kufungua kampuni za ujenzi wa barabara zinazotumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi yaani “**SPECIALIST CIVIL WORKS-LABOUR BASED CONTRACTORING FIRMS”** kisha kupata sifa za kisheria

za kununua kazi za miradi ya ujenzi au ukarabati wa barabara zinazotolewa na TARURA au TANROADS.

## 5. WALENGWA WA MAFUNZO:

a) Wahandisi wote wa barabara kutoka sekta ya Umma na binafsi,
b) Mafundi Sanifu wa barabara kutoka sekta ya Umma na binafsi,
c) Wasimamizi wa Miundombinu (Estates Managers) toka taasisi mbalimbali za Umma na Binafsi,
d) Makandarasi wenye nia ya kujenga au kuimarisha uwezo wa kazi zao za matengenezo/ ukarabati wa barabara kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi na,
e) Watu binafsi wenye uzoefu katika kazi za barabara au majengo na wanaohitaji kujiendeleza na kujifunza zaidi kazi za barabara.

## 6. LUGHA YA MAFUNZO:

Lugha itakayo tumika katika kozi ya ukarabati na matengenezo ya barabara ya changarawe/udongo itaendeshwa kwa kutumia mchanganyiko wa lugha ya Kiingereza na Kiswahili.

## 7. ADA ZA USHIRIKI

Mshiriki atapata huduma za chakula na malazi zinazotolewa na Taasisi kwa gharama ya ada kiasi cha Tsh. 1,600,000.
Ada ya ushiriki ilipwe kwa kutumia '**Control Number**' itakayotolewa kwa mtu atakayehitaji mafunzo kwa kuwasiliana na uongozi mapema kabla ya kozi kuanza. Inashauriwa kuwa ada ilipwe angalau wiki mbili kabla ya kozi kuanza.

## 8. NAMNA YA KUTUMA MAOMBI YA KOZI:

Wale wote watakao hitaji kujiunga na kozi tajwa hapo juu wanatakiwa kutuma maombi yao kwa kutumia anuani ya Posta au barua pepe zilizotolewa hapa chini au wanaweza kupiga simu kwa kutumia namba zilizotolewa kwa kupata maelezo zaidi.

## WASILIANA NASI


**MKUU WA TAASISI**
**TAASISI YA TEKNOLOJIA YA UJENZI**
**ICoT,**

**S.L.P 963,**
**MOROGORO.**
**Simu : 023- 2935229/023- 2935226**
**: 0692652881/0787059555**
**Nukushi : 023-2935227**
**Barua pepe : mwti@morogoro.net**

**S.L.P 1957,**
**MBEYA.**
**Simu : 025 295 7484/5**
**: 0764775354/0769317404/0765251509**
**Nukushi : 025 295 7486**
**Barua pepe : attimbeya@mow.go.tz,**
**attimbeyafrica@gmail.com**